# Wakulima, wafugaji waondolewa wasiwasi kuhusu viwango

**Na Mwandishi Wetu, Morogoro**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limesema limejidhatiti kuandaa viwango na kudhibiti bidhaa za kilimo na ufugaji, ikiwemo, mbegu, mbolea, viuatilifu, mashine za kulimia na vyakula vya mifugo.

Hayo yalisemwa wiki iliyopita na Ofisa Viwango wa shirika hilo, Mwajuma Iddi, wakati wa Maonesho ya Kilimo na Mifugo yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro.

Idd alisema shirika hilo ndiyo taasisi pekee ya kuandaa viwango na kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa nchini, hivyo wamejidhatiti kuandaa viwango na kudhibiti bidhaa za kilimo na ufugaji.

Alifafanua kwamba shirika hilo huandaa viwango kupitia kamati zake za kitaalamu zinazojumuisha wadau muhimu katika sekta husika, wakiwemo, wahadhiri wa vyuo vikuu, wazalishaji, wafanyabiashara, wadhibiti, watumiaji, wizara husika, wasindikaji na wengine.

Katika kutimiza majukumu hayo, Idd alisema TBS ina kamati tano katika sekta ya kilimo na ufugaji. Alitaja kamati hizo kuwa ni Kamati ya mbolea (AFDC 10), Kamati ya viuatilifu na vichafuzi katika vyakula na kilimo (AFDC 27) na Kamati ya mbegu (AFDC 30).

Nyingine kwa mujibu wa Idd ni Kamati ya mashine za kilimo (GDTC 5) na Kamati ya vyakula vya wanyama (AFDC 9).

"TBS pia ina kamati zingine za vyakula vitokanavyo na kilimo na mifugo (ufugaji) zenye lengo la kutengeneza viwango za bidhaa hizo," alisema na kuongeza;

"Katika mchakato wa kutengeneza viwango, wadau wote na jamii kwa ujumla hushirikishwa kupitia rasimu ya viwango yaani 'Draft Tanzania Standard for public comments' ambapo kiwango hutumwa kwa wadau na jamii kupitia tovuti ya shirika na barua pepe kwa wadau, wizara na tunapeleka na kuwataarifu Shirika la Biashara Duniani (WTO) ili waweze kuvituma viwango vyetu katika nchi zingine zitoe maoni yao visije kuleta vikwazo katika biashara katika utekelezaji viwango hivyo.

Aidha, alisema TBS pia hushikirikiana na taasisi zingine katika kudhibiti bidhaa katika kilimo na mifugo kama vile TPRI, TOSCI na nyinginezo lengo likiwa ni kuleta ufanisi katika kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa katika kilimo na mifugo.

Kwa upande wake Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu aliwataka wadau wa sekta ya kilimo na mifugo kujitokeza kushiriki katika uandaaji wa viwango vinavyohusiana na maeneo hayo.

Katika maonesho hayo, Mayugu alisema walitoa elimu kwa washiriki na wananchi kwa ujumla kuhusiana na masuala ya viwango, utaratibu wa kupata alama ya ubora ya tbs, umuhimu wa kudhibitisha ubora wa bidhaa zao na majukumu mapya yanayotekelezwa na shirika hilo kwa sasa, ambayo awali yalikuwa chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Majumu hayo mapya kwa TBS yanatokana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019 ambayo yameleta mabadiliko katika Sheria ya Viwango Na: 2 ya mwaka 2009.

Kufuatia mabadiliko hayo, majukumu ambayo awali yalikuwa chini ya iliyokuwa TFDA kwa sasa yanatekelezwa na TBS ni pamoja na usajili wa jengo, kusimamia masuala ya usalama na ubora wa chakula na vipondozi na upimaji wa bidhaa za vyakula na vipodozi kwa lengo la kudhibiti ubora.

Majukumu mengine ni utoaji wa leseni au cheti cha TBS kwa bidhaa za chakula na vipodozi na usajili wa bidhaa za vyakula na vipodozi vinavyotoka nje ya nchi.



RC Mbeya aonya

# Magufuli aanika mafanikio, mapato ya sekta ya uvuvi

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

RAIS John Magufuli, juzi alitumia Sherehe za miaka 58 ya Uhuru kuelezea mafanikio makubwa yaliyopatikana kupitia Sekta ya Uvuvi baada ya Serikali kuongeza mapambano dhidi ya uvuvi haramu na kuwezesha kuongezeka mapato kutoka sh. bilioni 379 mwaka 2016/2017 hadi kufikia sh. bilioni 691 mwaka 2018/2019.

Akizungumza kwenye maadhimisho ya Uhuru yaliyofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Rais Magufuli alisema mapambano hayo ya uvuvi haramu yamewezesha pia kuongezeka kwa mavuno ya samaki kutoka tani 387,547 mwaka 2017/2018 hadi kufikia tani 448,474 mwaka 2018/2019.

Rais Magufuli alisisitiza kuwa vita dhidi ya uvuvi haramu imewezesha sasa wakazi wa mikoa inayozunguka Ziwa Victoria kuanza kupata samaki wakubwa hali iliyowezesha ongezeko kubwa la mapato ya nchi yatokanayo na sekta ya uvuvi.

"Tumeongeza pia mapambano dhidi ya uvuvi haramu hali ambayo imesaidia upatikanaji wa samaki.. Kwa mfano kwenye mwaka 2018/2019 tulivuna tani 448,474 kutoka tani 387,547 mwaka 2017/2018," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisisitiza kuwa hata wananchi wa mikoa inayozunguka Ziwa Victoria ni mashahidi wa mafanikio hayo ya operesheni za kupambana na uvuvi haramu kwani nao wanashudia ongezeko la samaki.

"Lakini hata ninyi wana Mwanza ni mashahidi hivi sasa kwa mikoa hii ya Mara, Mwanza na Kagera kwamba samaki wakubwa wameanza kupatikana hii pia imesaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka bilioni 379 mwaka 2016/2017 hadi kufikia sh bilioni 691 mwaka 2018/2019," alisema Rais Magufuli.

Pia Rais Magufuli alisisitiza kuwa kwa kutambua kuwa takribani asilimia 65 ya Watanzania wanajihusisha na shughuli za Kilimo Uvuvi na Ufugaji Serikali imefuta zaidi ya tozo 100 kwenye sekta hizo.

Mbali na mafanikio hayo ya Operesheni za kupambana na Uvuvi haramu, Rais Magufuli pia alisema awamu ya tano inaendelea kutatua migogoro ya ardhi ili kuwawezesha wananchi kuendelea na shughuli za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa ufanisi mkubwa.

"Tunashughulikia pia migogoro ya ardhi ikiwemo kuviruhusu vijiji 920 vilivyokuwa kwenye maeneo ya hifadhi kuendelea kuwepo" alisisitiza Rais Magufuli.

Wakizungumza kwenye viwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza baadhi ya wakazi wa mikoa inayozunguka Ziwa Victoria wamekiri kuwepo ongezeko kubwa la samaki kutokana na usimamizi madhubuti wa Serikali kwenye rasilimali hizo.

Mmoja wa wananchi wa Mwanza Gaudensia Maduka alisema kabla ya Rais Magufuli kuingia madarakani walikuwa wananunua samaki kilo moja kwa sh 7,000 lakini kutokana

**Kaimu Meneja Wakala wa Vipimo Mkoa wa Temeke, Krishna Mahamba akieleza jambo kwa waandishi wa**



# Vijana kunufaika mtandao uvuvi, mifugo

Na Mwandishi Wetu

VIJANA kutoka mikoa 13 ya Tanzania Bara na visiwani wanatarajiwa kunufaika na mtandao wa vijana unaojihusisha na shughuli za uvuvi na mifugo.

*Kuanzishwa kwa mtandao huo, kutawasaidia vijana nchini kujiajiri moja kwa moja kupitia kwenye sekta ya uvuvi na mifugo.*

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mtandao huo, uliofanyika jijini hapa, Rais wa mtandao huo, Laban Boaz, alisema vijana chini ya miaka 35, kutoka mikoa mbalimbali watanufaika na mtandao huo kwa kufundishwa mbinu bora za kisasa za ufugaji.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo, ni kuhamasisha vijana kujiajiri katika sekta ya mifugo na uvuvi kwa kutumia njia za kisasa ambazo zitasaidia kuongeza uzalishaji mali na ajira kwa vijana.

Laban alisema kilichofanya kuanzisha mtandao huo, ni baada ya kuangalia mwanya uliopo kati ya wazee na vijana.

"Mtandao huu utasaidia kuwapa ujuzi na maarifa namna ya kufuga kisasa na vijana waliopo vijijini ambao walikuwa hawafikiwi na maarifa hayo na lengo ni mtandao huo kuwanufaisha vijana," alisema Laban.

Alisema mtandao huo uliananzishwa jijini Dar es Salaam mwaka 2017, lengo likiwa kupanua wigo wa vijana nchini.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde, alisema mtandao huo ni juhudi za muda mrefu ambazo zimefanywa na Umoja wa Afrika kupitia mradi wa kuendeleza rasilimali za wanyama (AU-IBAR).

Alisema hilo limewashirikisha vijana wanaojihusisha na kazi tofauti katika mnyororo wa thamani ya mifugo, samaki, kuku na nguruwe na kupitia mtandao huo watawekwa kufanya kazi ya mnyororo wa thamani.

Nandonde alisema serikali itaendelea kushirikiana na mtandao huo, kuwafikia vijana ili waitumie fursa hiyo ipasavyo.

Makamu wa Rais wa mtandao huo, Veronica Lyambiko, alisema wamefikia hatua ya kuanzisha mtandao huo, kwa kuwa vijana wengi nchini wanakabiliwa na tatizo la ajira.

Alisema, kupitia mtandao huo, idadi ya vijana wataingia na kuwafikia vijana vijijini.

Scanned by CamScanner